

Kuku 101

-Usimamizi wa
Ufugaji wa Kuku
katika Jamii
Zinazoendelea

Na

Jon Moyle, Ph.D.
UNIVERSITY OF
MARYLAND
EXTENSION



Yaliyomo

Utangulizi.....	3
Sehemu za Nje za Kuku.....	5
Kuanza.....	6
Mambo ya Msingi ya Ufugaji wa Kuku.....	16
Kuhusu Joto la Kuku Jike (Koo).....	25
Mifano ya Kimo cha Chombo cha Kulishia Kuku.....	28
Mifano ya Kimo cha Chombo cha Kunyweshea Maji.....	30
Kuku wa Mayai na Wazalishi (wa nyama).....	39
Kuatamia Mayai.....	45
Kutumia Kuku Jike Kuatamia Mayai.....	48
Kuchagua Kuku Wazalishi (Kuku wa Mbegu).....	53
Kuchagua kuku wa Nyama.....	58
Kuchagua Kuku wa Mayai.....	61
Kubainisha Kuku Wazuri Wanaotaga.....	65
Kuwalisha Kuku.....	72
Magonjwa ya Kuku.....	85
Baadhi ya Magonjwa ya Kuku Yanayofahamika.....	94
Chanjo.....	115
Bioulinzi.....	119
Kutunza Kumbukumbu	133

Kuku wa Kisasa

Kuku wanapatikana duniani kote, na wana ufanisi katika kumeng'anya chakula na kuwa protini ya ubora wa juu

Protini ya ubora wa juu ni muhimu kwa ajili ya ukuaji wa kawaida wa mtoto.

Kuboresha ufugaji wa kuku sio tu huongeza usalama wa chakula na lishe bali pia huongeza uhakika wa kipato.

Wastani wa matumizi ya nyama ya kuku duniani ni takribani kilogramu 13.2 kwa mtu mmoja kwa mwaka.

Kuku wa kisasa wanaweza kufikia uzito unaokubalika kwenye soko ndani ya miezi 3.

Wanabadilisha chakula na kuwa nyama kwa ufanisi.

Wastani wa matumizi ya mayai duniani ni takribani kilo gramu 8.9 kwa mtu mmoja kwa mwaka.

Leo kuku mmoja wa mayai anaweza kutaga mayai 300 kwa mwaka.

Maganda ya mayai yapo yenye rangi nyingi ikiwa ni pamoja na: nyeupe, kahawia, bluu na rangi ya mzeituni.

Rangi ya ganda la yai haiathiri ubora wa yai.

Kwa sababu gharama za kuanzisha na kuendesha zipo chini pamoja na kuwa na uwezekano mkubwa wa kuboresha maisha ya watu, ufugaji wa kuku ni moja ya sehemu ya kuanzia katika biashara za kilimo duniani.



Aina za Ufugaji Kuku Zinazofahamika Katika Jamii Zinazoendelea

Ufugaji Huria

Kuku wanajitafutia chakula wenyewe

Kuku wa kienyeji wanayamudu vizuri mazingira haya



Ufugaji nusu shdidi (nusu kisasa)

Kuna udhibiti kiasi wa banda na chakula.

Kuku wa kienyeji, kuku wa kisasa au mchanganyiko wa aina hizo mbili wanayamudu vizuri mazingira haya.

Ufugaji shadidi (kisasa)

mdogo/wa kati Kuku wanafungiwa ndani Chakula kinadhibitiwa Kuku wa kisasa au walioboreshwa wanayamudu vizuri mazingira haya



Aina za Kuku

Kuku wa Nyama

Ni wazuri katika kuzalisha nyama lakini hawana ufanisi katika uzalishaji wa mayai



Kuku wa Mayai


Ni wazuri katika uzalishaji wa mayai lakini hawana ufanisi katika uzalishaji wa nyama Hawahitaji majogoo ili watage mayai



Kuku wa

Nyama Wanazalisha nyama pamoja na mayai lakini Mavai kwa kiwango cha chini

Sehemu za Nje za Kuku



Kuanza



Hatua za Kwanza

Shughulika na kuku wako kama biashara

Andaa Mpango wa Biashara

Kwa nini unataka kuongeza
uzalishaji? Je, unajua utakwenda
kuuza wapi kuku wako?
Soko lako lipo wapi?
Wateja wako wanataka nini?

Tunza kumbukumbu

Hii itakuwezesha kuona iwapo unapata pesa au la
Husaidia kubainisha kuku bora zaidi ili waweze kutumika
kama wazalishi (mbegu) Wtunze kuku wale tu
wanaoweza kuzalisha

Fahamu kuku wako wanatoka wapi

Wanunue kutoka kwa mfugaji mzuri ambaye anawatunza vizuri kuku
wake
Je hao kuku wamepewa chanjo?
Epuka kununua kuku sokoni

Wanaweza kuleta ugonjwa mwingi kwenye kuku wako

Watenge kuku wako wapya uliowanunua na kuku wako wa sasa
kwa kipindi cha wiki 2 hadi 3 ili kuhakikisha kwamba hawana
magonjwa.

Andaa kila kitu kabla hujanunua kuku wako.



Kuanza

Kuku wanahitaji mambo matatu ili
waweze kukua Ulinzi (banda)

Dhidi ya mazingira

Dhidi ya wanyama

wala kuku

Chakula

Maji



Chicks need more
protection from the
environment than adult
birds



Banda la Kuku

Hakuna banda la kuku ambalo ni "kamilifu".

Ili mradi tu mahitaji ya kuku yamefikiwa, basi takribani kila aina ya banda inaweza ikawa ni nzuri.

Mabanda yanapaswa kujengwa ili:

Yakidhi mahitaji ya kuku


Kuwalinda dhidi ya mazingira na wanyama wala kuku. Kumwezesha mfugaji kuwapatia mahitaji yao.

Kukausha vizuri maji na maji hayatuami.

Yanawezesha hewa kuzunguka kwenye banda

Chini ya miti mirefu ambayo inaweza ikatoa kivuli katika maeneo ya joto

Hata kuku wanaofugwa katika mazingira huria wanaweza kunufaika na mabanda, kwa kuwa kuku hao wataweza kuepuka hali ya hewa mbaya na kutafuta usalama dhidi ya wanyama wala kuku, hususani wakati wa usiku ambapo matukio mengi ya kuliwa kuku hutokea



Mfumo mbaya wa
kukausha maji



Mfumo mzuri wa
kukausha maji

Kutengeneza Banda

Katika maeneo makavu:

Mabanda ambayo yanapitisha hewa kwa asili huhitaji kuwekwa eneo ambalo litaruhusu upepo kuzunguka ndani.

Jaribu na lielekeze banda mashariki magharibi ili kuzuia mwanga wa jua wa moja kwa moja kutua kwenye kuku.

Sehemu za wazi zinapaswa kuruhusu hewa nyingi kuweza kuingia katika banda kadri iwezekanavyo

Miti mirefu ambayo inaweza kuweka kivuli kwenye badanda lakini isiweze kuziba upepo unaovuma inaweza kusaidia kupunguza makali ya joto.

Mabanda yanapaswa kuwa mbali-mbali ili kwamba banda moja lisiweze kuzuia upepo kuvuma kwenda kwenye banda jingine

Mabanda yanapaswa kuwa na paa refu.

Mapaa mafupi yanaleta ugumu katika kufanya kazi

Mapaa marefu pia husaidia ndege kupoza joto kwa kuruhusu hewa ya joto kutoka.

Tumia zana zinazopatikana katika eneo lako, na ukuta na sakafu inapaswa kuwa laini ili kuwezesha mchakato wa kufanya usafi kuwa rahisi

Kwa hali ya hewa ya baridi, mapazia yanayoweza kushushwa na kupandishwa kwenye madirisha na sehemu zinazopitisha hewa, yataruhusu banda kufungwa wakati ambapo hali ya hewa ni mbaya, au ni baridi sana kuku kuweza kustahimili

Mabanda yanayotumika kufugia vifaranga yanapaswa kuwa na uwezo wa kuziba upepo wanapokuwa wadogona halafu kufunguliwa kwa ajili ya kuku wakubwa (tumia mapazia yanayoweza kufunguliwa na kufungwa).



Kutengeneza Banda

Weka urefu wa kutosha wa paa kutoka ukuta unapoishia ili kuzuia maji kuingia ndani mvua inaponyesha. Hakikisha kwamba maji yanakauka haraka sana kutoka kwenye banda

Hakikisha kwamba banda limejengwa kwa namna ambayo wanyama wala kuku hawawezi kuwafikia kuku.

Kuna aina kuu mbili za mabanda

1. Bada la kufungiwa - kuku wapo ndani muda wote
2. Banda ambalo kuku wanalala usiku tu – Kuku wanaachiwa kwenda kujitafutia chakula wakati wa mchana. Hatari ya magonjwa inaongezeka kuku wanapotoka nje. Wanakutana na kuku na ndege wengine.

Wanaweza kuingiliana na ndege wa porini na kutengeneza hatari ya magonjwa

Kuku wanaweza kukutana na wanyama wala kuku (ikiwa ni pamoja na wizi unaofanywa na majirani) wanapokuwa nje.

Kuku wanaweza kupata sehemu ya chakula cha ziada kwa kujitafutia chakula cha mbegu na wadudu.

Ukadiriaji wa uzito (kiwango cha juu)

(Kwa kuku wanaofugwa na wanaruhusiwa kutoka nje, ni sawa kwa wiki 3 za mwanzo)

Umri (Wiki)	Wiki 0 – 2	Wiki 2 – 5	Wiki 6 - Waliokomaa
Kuku / mita ya mraba	30	20	5*
Kuku / futi za mraba	4	1-2	1/2

***Kuku wakubwa watahitaji nafasi zaidi kuliko kuku wadogo.**

Banda




Birds are maintained indoors all the time





Kuzungushia fensi kwenye banda la kuku wako ili kuzuia kuku wa jirani kuchangamana na kuku wako husaidia kuzuia magonjwa

Banda



Banda la Kuku

These structures lacks window to allow for ventilation
Poor design



Kuku wanaojitafutia chakula wenyewe
watahitaji kivuliili kuwakinga na jua na
kuwafanya wajihisi
salama

Banda la Kuku - Matandiko

Matandiko yanasaidia ikiwa kuku wanafugiwa kwenye banda wakiwa wamefungiwa, yanafyonza unyevu, yanafanya kazi kama kochi kwa kuku, na hupunguza makali ya kinyesi cha kuku.

Vigezo vya kuangalia:

Lazima yawe na
uwezo wa kufyonza
maji Mepesi Yasiyo
ya Gharama

Yasiwe na sumu (yasiwe na kuvu/fangasi)

Lazima yawe na uwezo wa kutumiwa katika matumizi mengine baada ya kutumika, kwa mfano, mboji, mbolea au nishati (kuweza kupikia)

Zana kama vumbi ya mbao, randa za mbao, mabua, pumba za mpunga na maganda ya karanga ni zana nzuri za kutengenezea matandiko ya kuku.

Tumia matandiko bora zaidi kwa vifaranga.

Tumia matandiko safi kwa ajili ya viota na halafu yakishachafuka, yahamishie

kwenye sakafu. Jitahidi kuhakikisha kuwa matandiko yanakuwa makavu muda wote.

Ikiwa eneo ndani ya banda litapata unyevu, badilisha matandiko na weka makavu.

Ikiwa matandiko yamelowana yafute maji ili kukausha mahali palipolowana

Sio lazima kupasafisha na kuweka matandiko makavu hadi utakapokuwa tayari kuanza kufuga kundi jingine la vifaranga, hata kama utanza na kuku wa mayai usiyabadilisha hadi yatakapofikia umri wa miezi 18 au zaidi.

Matandiko kwenye banda lako yawe na ujazo wa sentimita 7.5 (inchi 3) kutoka chini

Matandiko makuukuu yanaweza kuuzwa kama mbolea au mboji

Pumba za Mpunga



Maganda ya Msonobari



Majani Yaliyokatwa



Mambo ya
Msingi katika
Ufugaji wa
Kuku



Vifaranga Bora

Chukua mbegu bora kabisa kadri iwezekanavyo

Jaribu aina tofautitofauti ili kujua ni aina ipi inafanya vizuri katika eneo lako.

Jaribu kununua vifaranga kutoka kwa wauzaji tofautitofauti. Ikiwa unayenunua kwake sasa hana vifaranga wazuri nenda kwa mwingine.

Vifaranga bora wanapaswa kuwa:

Mkavu na manyoya marefu chini. Macho yanapaswa kuwa angavu na mazima. Awe mchangamfu

Kitovu kinapaswa kuwa kimekauka kabisa.

Miguu inapaswa kuwa angavu na miororo.

Asiwe na kilema chochote



Vifaranga Wenye
Ubora Mzuri



Vifaranga Wasio na Ubora

Usafirishaji wa Vifaranga

Hakikisha kwamba vifaranga wanasafirishwa vizuri.

Kifaa kinachotumika kuwasafirisha kinapaswa kuwa na uwezo wa kupitisha hewa nyingi.

Kusiwe na joto sana au baridi sana 22 - 28 oC (70 – 82oF)

Usiwaache wanapoweza kufikiwa na mwanga wa jua moja kwa moja

Hakikisha kwamba mahali walipowekwa kuna nafasi ya hewa kuzunguka ndani.

Tabia inayoonyeshwa na kifaranga wakati wa kusafirisha ni kiashiria kizuri cha dalili ya tatizo wakati wa kuwasafirisha:

Katika hali ya kawaida, kifaranga wa siku moja anapumua kimya kimya kupitia pua zao, wanapoteza maji kidogo tu.

Wanagawanyika kwa usawa kwenye masanduku, wanapiga kelele kidogo na wanakuwa si wachangamfu kiasi.


Wakati wa joto, vifaranga wanapanua midomo yao na kuhema, ambapo maji yanatoka kwenye mapafu yao na mifuko ya hewa ili kuwasaidia kutuliza joto.

Hii itasababisha vifaranga kupoteza maji.


Halafu vifaranga wataanza kupiga kelele.

Wafungue vifaranga mara moja utakapowasili kwenye banda lako. Waingize ndani na watoe kwenye kifaa ulichowabebea.

Usiache kwenye banda vifaa vya zamani ulivyotumia kubebea vifaranga.



Hatua za Ukuaji



Uanguaji

Wiki mbili za mwanzo za uhai

Vifaranga kuendelea kuishi hutegemea ni haraka kiasi gani wanazoea mazingira ya kwenye banda na huu ni muda muhimu sana kwa kundi hili, wakulima wanapaswa kutumia muda mwingi zaidi pamoja na kuku wao.

Makosa yaliyofanywa wakati wa vifaranga yanaweza yasirekebishwe na yanaweza kuathiri ukuaji wa kuku wako.

Hali ni hiyo hiyo kwa aina zote za kuku, kuku wa mayai, kuku wa nyama na broila.

Mambo 6 ya Msingi Kuhusu Vifaranga

1. Maandalizi
2. Udhibiti wa Joto
3. Usimamizi wa Chakula
4. Usimamizi wa Maji
5. Usimamizi wa Mwanga
6. Ubora wa Hewa/Mzunguko wa Hewa




Pre-Placement means having everything ready for the birds when they arrive

- House is clean and warm
- Heaters are running
- Feed and water are ready and placed in the house for the birds



Mfano wa jinsi ya kuweka chakula na maji (suala muhimu ni kuwa na chakula kingi na maji)



While birds are often brooded in “brooder rings” it is not necessary to use perfect circles. Chickens can be brooded in almost any room (or shape) as long as they are protected from the environment and have access to heat, food and water, brooder rings are not necessary, whole rooms/barns can be used to brood as long as temperature is maintained and food and water are available.

Joto

Before the chicks arrive, make sure everything is prepared
Litter should be warm and dry
(~33°C, 92°F)


Chanzo bora cha joto ni cha lazima ili vifaranga wapate joto. Chini ya kanopi au kuning'iniza - huelekeza joto chini karibu na vifaranga. Tumia zana uzlizonazo

Vyanzo vya joto vya umeme, mafuta, mkaa, na gesi ni aina zilizozoeleka.

Mnunuzi kutoka kwenye taa ya miale unavipatia joto vitu ulivyovimulika; hauipatii joto hewa.



Be careful not to let the litter/bedding under the heat source get too hot as it can result in a fire



Joto

Joto kwa kiwango cha kifaranga linapaswa kuwa takribani 34° C (94°F) karibu na chanzo cha joto na sehemu ya kutuliza joto ikiwa umbali wa mita 1 (futi 3).

Kabla hujawaleta vifaranga hakikisha kwamba chanzo cha joto

kinafanya kazi vizuri. Je, vifaranga wana joto sana au baridi sana?

Mara kwa mara kagua kwa kutazama na kagua joto kwa kutumia themometa mara moja moja.

Kagua joto mara kwa mara wakati wa hali ya hewa ya joto sana au baridi sana.

Unapowaweka vifaranga - joto la kiwango cha kwenye sakafu kiwe 33-34°C (90- 92°F) kwa siku kadhaa za mwanzo kisha taratibu punguza joto kwa takribani 2.5°C (5°F) kwa wiki.

Mara vifaranga watakapoanza kuota manyoya vizuri, joto linaweza kushuka kwa haraka, na kutunza nguvu.


Mzunguko mzuri wa hewa ni muhimu sana huku joto sahihi

likidumishwa. Banda linapaswa kuwa na mwanga na kuruhusu hewa kupita bila vizurizi.

Kusiwepo na harufu kali ya amonia.


Hewa haipaswi kuwa na unyevu sana.

Hewa yenye unyevunyevu mwingi inaweza kufanya banda kuwa la unyevu na kuku kuwa na afya mbaya.





Mifano ya Vyanzo vya Joto


Joto Zuri



Baridi



Joto



Upepo mwanana

Chakula/Malisho na Maji

Chakula na maji vinapaswa kuwa tayari wakati wote vifaranga wanapoletwa. Kama vipo waanzishie vifaranga vyakula laini.

Hakikisha kwamba kuna vifaa vya kulishia na kunyweshea maji vingi ili vifaranga waweze kuvifikia kwa haraka na kwamba kuna nafasi ya kutosha kuwawezesha wote kula.



Weka baadhi ya chakula chako karibu na chanzo cha joto.

Tumia kile ulichonacho, usitumie pesa kwenye vifaa vya gharama kubwa ikiwa wewe huna uwezo wa kuvimudu

Mwazi unaweza kutumika kutengeneza vyombo vya kulishia na kunyweshea maji. Makopo ya mafuta ya kupikia yanaweza kukatwa na kutengeneza vyombo vya kulishia na kunyweshea.



Use extra feeders for the first couple of days to help chicks get off to a good start



Chakula/Malisho na Maji

Unapowaweka vifaranga kwenye banda waweke kwenye chakula (inakuwa rahisi kwao kukifikia chakula).

Weka karatasi kwenye sakafu, halafu zifunike kwa chakula, kisha waweke kuku hapo. Ziondoe karatsi baada ya siku kadhaa.

Kwa wiki ya kwanza, jaza kabisa vyombo vya kulishia.

Wiki ya pili punguza viwe robo tatu na baada ya hapo chombo cha kulishia kisijae ziadi ya nusu. Hii inawafanya kuku wasiharibu chakula.


Kimsingi, vyombo vya kulishia vingi katika kila banda ni bora zaidi. Hupaswi kuacha kuku watafute chakula



Chakula/Malisho na Maji

Waangalie kuku wakila na hakikisha kwamba wote wanakifikia chakula.

When chicks are placed, the feeder needs to be low enough so the chicks can walk in it
As they grow, raise the feeder so that the chicks can eat while standing (mid chest height)
Look at the smaller birds when adjusting the feeder height



Mifano ya Kimo cha Vyombo vya Kulishia

Kwa
Wiki ya
Kwanza



Wakati
Wanakua



Wakubwa



Chakula na Maji

Kwa wiki chache za mwanzo, vifaranga wanahitaji chakula chenye ubora mzuri watakachoanza kula kikiwa na protini ya kiwango cha asilimia 18-22% (watalishwa katika kipindi chote wanachokua kuvuka hatua ya vifaranga).

Baada ya hapo wanaweza kulishwa kiwango cha kuku wanaokuwa cha takribani asilimia 18% ya protini hadi watakapokua.

Kwa kuku wa mayai lische ya protini ya asilimia 16% inatosheleza kabisa. Hakikisha kuku hawakosi chakula!

Watachelewa kukua.

Wanahitaji chakula kingi ili wakue

(ni gharama zaidi). Hakikisha vifaranga

hawakosi maji!!!

Tumia maji safi tu ambayo wewe unaweza kunywa.

Vyombo vya kunyweshea maji vinapaswa kusafishwa kila siku.

Inaweza kusaidia ikiwa utachomeka mdomo wa kifaranga kwenye maji ili kujua yalipo, hususani baada ya safari ngumu.

Ikiwa vifaranga watatumia zaidi ya siku moja wakisafiri kupelekwa kwenye banda, wapatie kwanza maji kwa masaa kadha kabla ya kuwapatia chakula.

Hii huwafanya vifaranga kuongeza maji mwilini

Kuku wenye njaa



Kuku walioshiba



Kimo cha Chombo cha Kunyweshea

Kwa vifaranga wadogo, weka chombo cha kunyweshea katika kimo cha chini hadi watakapojifunza kuyatafuta na kunywa.

Pandisha juu vyombo vya kunyweshea kadri kuku wanavyokua.

Rekebisha kimo kulingana ukubwa wa kuku.

Ikiwa ni kuku wakubwa basi vyombo vya kunyweshea pia vinapaswa kupandishwa juu, ikiwa ni wadogo basi vyombo vinapaswa kushushwa chini.

Mifano ya Kimo cha Vyombo vya Kunyweshea Maji

Kwa
Wiki ya
Kwanza



Wakati
Wanakua



Wakubwa



Kimo cha Chombo cha Kunyweshea Maji

Kwa kuku wanaokua, chombo kinapaswa kuwa kimo cha usawa wa kifua cha kuku.



Kwa kuku wakubwa chombo kinapaswa kuwa kimo cha usawa wa mgongo wa kuku jike.



Mifano Mizuri ya Chakula na Maji



Kukua

Kuku wanaokua huanzia mwisho wa kuwa vifaranga hadi wakati wanavunwa au wamekomaa kuweza kupandana.



Kukua



Usimamizi wake si mgumu sana.

Kuku wanaokua wanaweza kudhibiti joto lao la mwili.

Lakini bado wanahitaji joto la ziada hadi watakapokua na manyoya mwili mzima.

Watakapokua wakubwa wanaweza kukabiliana na hali ya hewa ya baridi bila tatizo ikiwa hawatalowana na hawatakaa kwenye upepo.

Ni bora zaidi kuwafungia ndani ya banda hadi watakapokuwa na wiki 4.

Vifo katika umri huu ni kidogo kwa kuwa kuku wanajua kutafuta chakula na maji.

Ili kuku waweze kukua harakaharaka hawapaswi kuishiwa chakula.

Kimo cha chombo cha kulishia kinapaswa kurekebisha kwa kipindi kadri

kuku wanavyokua. Ikiwa chombo cha kulishia kipo chini sana watamwaga chakula chini na hivyo chakula kupotea.

Hakikisha kwamba kuna nafasi ya kutosha kwenye chombo cha kulishia kwa kuku wote kula kwa wakati mmoja.

Ni muhimu kwamba maji yawepo muda wote.

Katika siku za joto, maji kukosekana yanaweza kusababisha kifo. Maji yanatakiwa kuwa safi na yasiyo ya chumvi.

Kuku wanakunywa maji mara mbili zaidi kadri wanavyokula.

This waterer is too low for adult birds, but good for young
If you have both large and small birds together set feed and water at the correct height for the smallest birds



Zuia Upotevu wa Chakula


Unapoleta vifaranga, weka vyombo vya chakula katika kimo cha chini kadiri iwezekanavyo.

Kisha taratibu vipandishe kadiri wanavyokua ili kusaidia kuzuia mabaki kuingia kwenye chakula.

Kiwango cha chakula kweye chombo cha kulishia kinapaswa kuwa kingi wakati kuku bado wadogo na kiwe kidogo wakati kuku wamekua wakubwa ili kuzia upotevu wa chakula.



Feeders are too low, and birds are wasting feed



Fix broken or damaged feeders to prevent wasting feed




Vitulio (vya ndege)

Husaidia kuwazuia kuku kukaa kwenye vyombo vya kulishia na vya kunyweshea. Husaidia kuepusha kinyesi cha kuku kungia kwenye chakula na maji.

Huweza kusaidia kuboresha uimara wa mifupa.

Perches can be made with locally available materials
If using branches, remove bark as it provides a place for parasites to hide



na kuvichafua Kukosekana kwa vitulio husababisha kuku kupanda kwenye vyombo vya kulishia na kunyweshea

Wanyama walao kuku



Vifaranga ni rahisi sana kushambuliwa na wanyama wala kuku.

Orodha ya wanyama wala kuku ni ndefu, badhi yake ni pamoja na:

Paka na mbwa, ni wanyama wa kufugwa lakini ikiwa hawatasimamiwa vizuri wanaweza kuwaona kuku kama chakula chao.

Panya

Bundi Wanyama

wa porini

Kicheche, fungo, paka pori, mbweha, nyoka, mwewe, kipanga na kadhalika.

Matukio ya kuku kuliwa na wanyama mara nyingi yanatokea usiku kwa hiyo hakikisha kwamba kuku wako wamo kwenye banda lao na hakikisha banda limefungwa kwa usalama.

Wafunike vifaranga kwenye masanduku au kwenye madumu ya chakula kwa waya ili kuwalinda.



Matatizo ya Kitabia

Wakati fulani kuku wanaweza kuonyesha
tabia zisizo za kawaida. Kula mayai
Akiendelea sana itakuwa vigumu
kumzuia. Kuku Kuwala Wenzie

Hii inaweza kuwa ni ishara ya tatizo
fulani. Ukosefu wa lishe kamili.
Amechoshwa na mazingira.
Kuna kuku mwenye jeraha.

Kukata mdomo kunaweza kufanyika ili kusaidia kuzuia au
kupunguza tatizo. Udonojaji wa manyoya
Ni sawa na kuku kuwala wenzie



Some feather loss is the result of mating,
(note feather loss on back as well as the
back of the head at the base of the comb)
May need to remove males at times to
allow hens to recover, be sure to allow
males access to females a couple of
times a week to maintain fertility
Reducing the number of males can also
help lessen the damage to hens, again
make sure there are sufficient males to
maintain fertility if eggs are to be
hatched



This hen needs her beak
trimmed to allow her to eat
properly
It can be done with a pair of
nail clippers

Kuku wa Mayai na wa Mbegu



Uzalishaji wa Mayai/Kuku wa nyama

Muda ambao kuku anachukua hadi kufikia wakati wa kupandana hutofautiana na aina ya kuku. Kwa kawaida huanza kutaga kuanzia umri wa wiki 18 hadi 22.

Aina nyingine zinaweza kuanza mapema zikiwa na umri wa wiki 16.

Aina nyepesi kwa kwaidia inakua haraka kuliko aina nzito.

Chakula na maji vinapaswa viwepo muda wote

Maji ni muhimu sana kwa kuwa ni sehemu muhimu ya yai.


Ikiwa maji ni adimu au hayapatikani kwa kipindi kirefu wakati wa mchana, uzalishaji wa mayai utashuka.

Banda ni lilelile kadri wanavyokuwa isipokuwa kwa viota vya kutagia.

Andaa sanduku moja la viota vya kutagia kwa kila kuku 4-6 lenye ukubwa wa 12x12x12 ni mzuri kwa kuku wenye ukubwa wa kawaida.

Andaa masanduku makubwa kidogo kwa kuku wenye umbo kubwa.

Weka viota kwenye eneo lenye gizagiza ili kuku waweze kuvutiwa kutaga mayai.



Uzalishaji wa

Majogoo si ya lazima ili kuku wa mayai atage.

Majogoo wanahitajika ili kurutubisha mayai na kuzaa vifaranga (jogoo 1 kwa majike 10 hadi 12).

Inachukua takribani masaa 24-27 kwa kuku jike kutengeneza yai na kutaga.

Kuku wanatumia kalisiamu kutoka kwenye mifupa yao ili kutengeneza maganda ya mayai, kalisiamu hii inapaswa ipatikane kwa njia ya chakula.

Vyakula vyenye kalisiamu ya chini hupunguza utagaji wa mayai na inaweza kusababisha kuku kuwa na mifupa dhaifu.

Kalisiamu pia inaweza kupatikana kwa kuwapa kuku konokono.

Inaweza kutumika badala ya unga wa nafaka kwa kuku wanaotaga.

Vipindi virefu vya hali ya hewa ya joto pia vinaweza kusababisha matatizo ya mifupa

katika kuku wa mayai wanaotaga sana.



Udhibiti Mwanga

Masaa 24 ya mwanga yanapendekezwa kwa siku 4
za mwanzo saa 20 za mwanga kwa siku 4-7.

Kwa wiki ya pili saa 16 za mwanga

Baada ya wiki ya pili mwanga wa asili unapaswa kuwa unatosha

Kimsingi, ikiwa mwanga unaweza kudhibitiwa kuku wanaweza
kukua kwa saa nane za mwanga baada ya wiki ya tatu hadi wafikishe
wiki 18 na kuwa na uzito unaofaa.

Udhibiti wa Mwanga (Pale Ambapo Hakuna Udhibiti wa Mwanga)

Umri (Siku)	Siku 1-4	Siku 4-7	Siku 8-14	Siku 15+
Kiwango cha Mwanga	Saa 24	Saa 20	Saa 16	Mwanga wa asili

If possible increase day length by at least one hour when birds reach
their 18-week body weight target
Use artificial light to create a constant day length of 14-16 hours to
encourage hens to lay the most eggs

Kuwaweka Kuku Wanaotaga katika Vizimba

Kuwaweka kuku wa mayai kwenye vizimba husaidia: Ndege wengi kuwekwa kwenye eneo dogo. Huwakinga na vimelea wa ndani. Upotevu wa mayai ni mdogo sana kwa sababu ya mayai machafu au kuvunjika. Kiwango cha chini cha vifo vya kuku. Bioulinzi ulioboreshwa.



Bird welfare may be a concern, especially if birds are crowded

Kuwaweka Kuku Wanaotaga katika Vizimba

Banda lenye ngazi mbili lililotengenezwa kwa mbao na waya na kufunikwa na turubai. Sakafu husafishwa na uchafu wa matandiko unatumika kama mbolea. Tumia kile ulichonacho/unachoweza kumudu.



These pens are large and allow the birds more freedom to move and has perches for the birds



Kuatamia Mayai



Kuangua Mayai

Yai linaanguliwa ndani ya siku 21, kuku ambao wanaatamia mayai na wanaolea vifaranga hawatagi mayai katika kipindi hicho.

Kutotolesha mayai kwa mashine hufanya kuku kuendelea kutaga.

Ili mayai yaweze kuanguliwa yanahitaji joto la

37.5°C (99.5° F).

Usiweka mashine za kutotolesha mayai sehemu ambapo zinaweza kupigwa jua moja kwa moja maana joto linaweza kuzidi.

Hakikisha kwamba mashine ya kutotolesha mayai ipo kwenye chumba kinachopitisha hewa vizuri na inalindwa dhidi ya mazingira.

Unyevunyevu sahihi ni 55, au 28.5 28.5°C (83°F)

Hakikisha kwamba vyombo vya kunyweshea vina maji ya kiwango kinachostahili, ili kuwepo na kiwango cha unyevunyevu kinachostahili.

Geuza mayai mara kwa mara, mara 4 hadi 8 kwa siku.

Baada ya siku 16 za kuatamia mayai hayahitaji kugeuzwa tena.



Kuangua Mayai



Wakati mashine nyingi za kutotolesha mayai zinatumia umeme, kuna baadhi ya mashine ambazo zinatumia mafuta ya taa.

Unapotumia aina hii ya mashine ni muhimu kuhakikisha kwamba moshi wa mashine unatoka nje ya banda.

Kama hakuna hewa ya kutosha kuweza kuutoa moshi nje, unaweza ukaongezeka na kuua kiinitete

kinachokua na kupunguza idadi ya vifaranga wanaoanguliwa.

Inaweza pia kusababisha matatizo ya afya kwa watu wanaoishi na kufanya kazi hapo.



Mfano wa mashine za kutotolesha

Jedwali la Utotoleshaji

Spishi (Aina)	Siku	Hali joto	Unyevunye vu
Kuku	21	37.5°C (99.5°F)	55-60
Bata	28	37.5°C (99.5°F)	55-60
Kwale	17-18	37.5°C (99.5°F)	55-60
Bata bukini	30	37.5°C (99.5°F)	60
Batamzinga	28	37.5°C (99.5°F)	55-60

Kutumia Kuku
Jike
Kuatamia
Mayai



Kutumia Kuku Jike Kuatamia Mayai



Ili kujua ni kuku yupi anaatamia mayai, angalia kuku ambao:

Muda wote wamekaa kwenye kiota, wanakataa kutoka kwenye mayai.

Anatimua manyoya na kukudonoa unapojaribu

kuchukua mayai. Hawana manyoya kwenye kifua.



Kutumia Kuku Jike Kuatamia Mayai

Waandalie sehemu salama kwa ajili yao ambayo inazuia wanyama wala nyama kuweza kuwala.

Weka karibu yao chakula na maji. Wapatie hewa ya kutosha.



Vifaranga wanapokuwa wadogo waweke mahali ambapo ni salama.

Wazungushie fensi wakati wa mchana ili wawe salama dhidi ya wanyama wala kuku.

Wakati wa usiku wafungie kwenye sehemu salama pamoja na mama zao kwa ajili ya kuwalinda.

Make sure food and water are accessible to the chicks when they hatch



Kuyatunza Mayai

Kusanya mayai mara 2-3 kwa siku.

Yatunze huku upande mkubwa wa yai
ukielekea juu.

Yatunze maya kwenye eneo tulivu la banda kwa ajili ya
kuatamiwa. Pasiwe pakavu sana au unyevunyevu
sana.

19-21 19 -21 °C ni joto bora zaidi.

Epuka kubadilikabadilika kwa hali joto, hakikishaa hali joto
haibadilikai. Usiyatunze sehemu ambapo yanaweza kupigwa na jua.

Yatunze mayai kwa siku 7 tu au chini ya hapo kabla ya kuyaweka kwenye
kuku ili yaatamiwe. Mayai kutoka kwa kuku kadhaa yanaweza kuwekwa
chini ya kuku mmoja.

Hii inakufanya kuweka mayai ambayo yalianguliwa wakati huohuo.



Kwa nini Mayai Mengine Hayaanguliwi?

Hayakurutubishwa.

Yalitunzwa kwa muda mrefu au yalitunzwa vibaya.


Yalikuwa machafu, ikiwa yai litavunjika na kufunika mayai mengine inaweza kuzuia yai lisipumue, mayai ambayo yamefunikwa kwenye uso ni nadra sana kuanguliwa.

Yanavunjika.






















Mayai yaliwekwa mahali ambapo mwanga wa jua ulikuwa unayafikia moja kwa moja.

Ikiwa mayai hayajaanguliwa subiri kwa siku kadhaa ili kuona kama yamerutubishwa.

Ili kujua kama yamerutubishwa fungua kwa makini upande mmoja wa yai na angalia kiinitete.




CHICK EMBRYO DEVELOPMENT

 <p>INFERTILE • No development.</p>	 <p>DAY 1 • Appearance of tissue development.</p>	 <p>DAY 2 • Tissue development very visible. • Appearance of blood vessels.</p>	 <p>DAY 3 • Heart beats. • Blood vessels very visible.</p>	 <p>DAY 4 • Eye pigmented.</p>	 <p>DAY 5 • Appearance of elbows and knees.</p>	 <p>DAY 6 • Appearance of beak. • Voluntary movements begin.</p>
 <p>DAY 7 • Comb growth begins. • Egg tooth begins to appear.</p>	 <p>DAY 8 • Feather tracts seen. • Upper and lower beak equal in length.</p>	 <p>DAY 9 • Embryo starts to look bird-like. • Mouth opening appears.</p>	 <p>DAY 10 • Egg tooth prominent. • Toe nails.</p>	 <p>DAY 11 • Comb serrated. • Tail feathers apparent.</p>	 <p>DAY 12 • Toes fully formed. • First few visible feathers.</p>	 <p>DAY 13 • Appearance of scales. • Body covered lightly with feathers.</p>
 <p>DAY 14 • Embryo turns head towards large end of egg.</p>	 <p>DAY 15 • Gut is drawn into abdominal cavity.</p>	 <p>DAY 16 • Feathers cover complete body. • Albumen nearly gone.</p>	 <p>DAY 17 • Amniotic fluid decreases. • Head is between legs.</p>	 <p>DAY 18 • Growth of embryo nearly complete. • Yolk sac is still on outside of embryo. • Head is under the right wing</p>	 <p>DAY 19 • Yolk sac draws into body cavity. • Amniotic fluid gone. • Embryo occupies most of space within egg (not in the air cell).</p>	 <p>DAY 20 • Yolk sac drawn completely into body. • Embryo becomes a chick (breathing in air cell). • Internal and external pip.</p>

COBB-VANTRESS, INC. • P.O. Box 1030 • Siloam Springs, AR 72761 • USA • Tel: 479.524.3166 • Fax: 479.524.3043 • info@cobb-vantress.com
COBB EUROPE LTD • Oyster House, Severalls Lane, Colchester, Essex, UK • Tel: +44 1206 835835 • Fax: +44 1206 756864 • info@cobb-europe.com
COBB-VANTRESS BRASIL LTDA. • Rodovia Assis Chateaubriand, KM 10 • CEP: 15110-000/Calça Postal 2 • Guapiçu-SP-Brasil • Tel: +55 (17) 3267 9999 • Fax: +55 (17) 3267 9992 • cobb.info@cobb-vantress.com.br
COBB-VANTRESS PHILIPPINES INC. • 5/F 8101 Pearl Plaza, Pearl Drive • Ortigas Center, Pasig City Philippines • Tel: +63 2 634 3590 • Fax: +63 2 634 3598

www.cobb-vantress.com

Kuchagua
Kuku wa
Mbegu (Aina
ya Kuku)



Vinasaba

Ukubwa wa mwili na kiwango cha uzalishaji ni tabia za kurithi.

Kwa kuku wa mayai - kadri kuku anapokuwa mdogo ndipo anataga mayai mengi - hahitaji chakula kingi kuweza kutaga mayai mengi.

Kwa kuku wa mayai - Aina ya Leghorn na Sex-link ni kuku wazuri kwa kutaga mayai mengi kwa kutumia chakula kidogo.

Kuku wa nyama wa kisasa wanakuwa haraka sana na kwa ufanisi mkubwa sana.

Kuku wa mayai,
kumbuka kuwa hawana
nyama nyingi.



Mchanganyiko wa kuku wa
kienyeji na wa kisasa.
Hawa kuku ni wa umri mmoja na
wanakula chakula kile kile, lakini
kuku wa kisasa ni wakubwa zaidi.

Uzalishaji wa Kuku


Kuku mara nyingi huwa wanachaguliwa kwa ajili ya ama nyama au mayai.

Hii ni kwa sababu ukichagua kwa ajili ya nyama husababisha kupungua kwa uzalishaji wa mayai na ufanisi wa kutaga mayai.

Pia, kama ukichagua kwa ajili ya ufanisi wa uzalishaji wa mayai, ukubwa wa mwili na misuli hupungua.



Ulinganishaji kati ya kuku wa kisasa wa nyama na kuku wa mayai kwa takribani wiki ya tatu ya umri wao, wanalishwa chakula kile kile na kutunzwa katika banda moja.



Mambo ya Msingi

Weka malengo ya munda mrefu.

Fikiri kwa kina ili kuweka malengo yako.

Tunza kumbukumbu vizuri.


Wafuatilie kuku wako.

Watunze wale ambao ni wazuri
zaidi na waondoe ambao ni wabaya.

Chagua kuku wenye afya pekee.

Usichague kuku wenye ulemavu wa mwili.

Utahitaji majogoo wachache tu kulinganisha na
majike. Jogoo 1 kwa kila majike 10.



Mambo ya Msingi

Mara zote walingenishe kuku wenye umri sawa.

Usiwalinganishe kuku wakubwa na kuku wadogo.

Umri wakati wa kuchagua inategemeana na aina ya kuku unaoawachagua na uwezo wao wa kuzalisha.



Kwa mfano, unaweza kuhitaji kuchagua kuku wa nyama akiwa na umri wa wiki 12 lakini kwa kuku wa mayai unaweza kusubiri hadi watakapoanza kutaga mayai.

Usiwalinganishe kuku ambao ni aina (mbegu) tufauti. Kuku wa nyama dhidi ya kuku wa mayai.

na



Chagua tu kuku wale ambao wana afya nzuri. Watenge kuku ambao wanapata ugonjwa.

Watenge kuku ambao hawaonekani wapo vizuri kimwili.


Chagua kuku ambao wana undu mwekundu angavu bila kuwa na madoa meusi.

Madoa meusi yanaweza kuwa ni kiashiria cha shida ya moyo.

Hakikisha kwamba wana macho safi angavu.



Kuchagua
Kuku kwa ajili
ya Nyama



Vigezo vya Kupima

Kiwango cha ukuaji - uzito.


Uwezo wa kubadilisha
chakula. Ukubalifu.

Afya.

Ukubwa wa

kuku

mkubwa



Kiwango cha Ukuaji - Uzito

Uzito ni rahisi kuupima na si jambo la kidhahania. Kuku wanaokua haraka huwa wanakuwa na ufanisi ziadi.

Kagua nyamanyama ili kuhakikisha kuwa anapokuwa misuli pia inaongezeka.

Mara zote hakikisha unapima katika umri ule ule.

Kwa mfano - umri siku 14 na 35.

Ubadilishaji wa Chakula

Hiki ni kipimo cha kujua ni kiasi gani cha chakula wanakula kwa kulinganisha na uzito wanaopata.

Kilo 3 za chakula na kupata kuku mwenye uzito wa kilo 1 ni sawa na uwiano wa ubadilishaji wa chakula wa 3 kwa 1.

Zoezi hili linaweza kufanywa kwa kuku mmoja mmoja (ni kazi ngumu kweli) au kwa makundi ya kuku (mara nyingi kuku wanapangwa kwa kuangalia wazazi wao ni akina nani, na wana umri gani).

Ukubalifu

Kuku wa nyama wanapaswa kuwa na mwili imara na uwezo mkubwa.

Angalia kuku ambao wana

Mgongo mrefu.

Kifua chenye kina

kirefu. Mwili mpana.

Angalia weye miguu mikubwa na muundi mpana.



Kuchagua Kuku wa Mayai



Vigezo vya Kupima

Uzalishaji wa

Mayai.

Ukubalifu.

Afya


Ukubwa wa Kuku Mkuba



Uzalishaji wa Mayai

Tumia kuku wako wanaotaga sana kama mbegu. Pima uzalishaji wa mayai.

Idadi ya mayai yaliyotagwa - tumia viota vilivyozungushiwa vyavu ili kujua kila kuku anataga mayai mangapi.



Trap nests work by preventing the hen from leaving until she is removed by a worker so they can identify which eggs she lays

Chagua kuku ambao wanaanza kutaga mayai mapema.

Chagua kuku ambao wanamzunguko mrefu wa kutaga, yaani, wanataga mayai kwa siku nyingi mfululizo kabla hawajaruka siku.

Watenge kuku ambao wananyonyoka manyoya mapema.

Kunyononoka manyoya – ni pale kuku wanapoacha kutaga na kupoteza manyoya yao. Chagua kuku wanaotaga mayai yenye ukubwa mzuri.

Watenge kuku wanaotaga mayai ambayo hayana umbo zuri.



Uzalishaji wa Mayai

Wachague kuku ambao hawaangui.

Kuku hawatagi mayai wanapokuwa wanaatamia.

Fanya hivi ikiwa tu una mashine ya kutotolesha mayai, au utakuwa unatumia kuku wengine kuangua mayai kwa ajili yako.

Ukubalifu

Kuku wa mayai wanahitaji uwezo wa kutosha ili kuendelea kutaga mayai mengi.

Angalia kuku ambao ni

Warefu

Wanene

Wenye uwezo mkubwa wa tumbo.

Pima kati ya mkuku na mifupa ya nyonga.



Afya

Chagua kuku wale tu ambao wana afya nzuri.

Watenge kuku ambao wana ugonjwa.


Hakikisha kwamba wana macho angavu safi.



Watambue Kuku
Wazuri
Wanaotaga



Mambo ya Kuangalia katika Kuku Jike



Kuku Asiyetaga



Kuku Anayetaga

Mambo ya Kuangalia katika Kuku Jike



Kuku Asiyetaga



Kuku Anayetaga



Kuku Anayetaga Vizuri



Kuku Asiyetaga Vizuri

Zingatia: Hii inafanya kazi kwa kuku wakubwa tu wenye miguu ya njano.



Kuku Anayetaga Vizuri



Kuku Asiyetaga Vizuri

Zingatia: Hii inafanya kazi kwa kuku wakubwa tu wenye miguu ya njano.

Pima kujua ni vidole vingapi vinaweza kutosha kwenye mifupa ya nyonga. Ikiwa vidole 3 au zaidi haviwezi kutosha basi huyo kuku hatagi. Vidole zaidi vikitosha ni bora zaidi.



Kuku Anayetaga Vizuri



Kuku Asiyetaga Vizuri

Pima kujua ni vidole vingapi vinaweza kutosha kati ya mkuku na mifupa ya nyonga.

Ikiwa vidole 3 au zaidi haviwezi kutosha basi huyo kuku hatagi.

Vidole zaidi vikitosha ni bora zaidi, pia panapaswa pawe laini si pagumu.



Kuku Anayetaga Vizuri



Kuku Asiyetaga Vizuri

Kulisha Kuku



Maji

Maji ni sehemu muhimu sana ya lishe ya kuku. Kuku wanahitaji kuwa na maji safi wakati wote.

Kuku hawawezi kutaga mayai ikiwa watakosa maji.

Tumia maji ambayo unaweza

kunywa. Maji machafu yanaweza

kusababisha kuku waugue.

Safisha vyombo vya kunyweshea kila mara.



Nzuri

Kuku wanaweza kunywa maji lakini hawawezi kuyachafua.



Mbaya

Maji yamechafuliwa na kinyesi pamoja na uchafu, chombo cha kunyweshea kipo chini sana na kuku wanaweza kupanda juu ya chombo cha kunyweshea. Ikiwa kuna vifaranga safisha mara kwa mara.

Kwa Nini Chakula

Afya bora

Mayai zaidi

Kuku wanakua haraka

A chalkboard with the title 'Equilibrer une' written at the top. Below it is a list of ingredients and their quantities:

Maïs	50
F. Poisson	20
T. Soja	5
T. D'arachide	5
T. Palmiste	10
Coquillage	10
Sel	0,5
Methionine	1
Premisc	2,5

Chakula chenye ubora mzuri kina virutubisho vitano.

1. Protini
2. Wanga
3. Mafuta
4. Madini
5. Vitamini

} Nishati (Nguvu)

Protini

Protini ni moja kati ya sehemu muhimu sana za chakula cha kuku. Ni muhimu kwa ajili ya ukuaji wa misuli na manyoya. Protini inaweza kupatikana katika:

Maharage - Soya, njegeera

Karanga

Samaki

Samaki na mifupa

Mashudu - ya ufuta, soya, mbegu za pamba, alizeti.

Wadudu

Majani ya moringa

Majani ya jamii kunde - maharage, kunde, muhogo (hadi 5%).

Mahitaji ya Protini na Nishati kwa Kuku wa Nyama

Umri (wiki)	0-3	3-6	6-8
Protini ghafi %*	22-23	20-21	18-20
Nishati kcal/kg	3,200	3,200	3,200

*Hutegemeana na ubora wa protini



Mahitaji ya Protini na Nishati kwa ajili ya Kuku wa Mayai

Umri (wiki)	0-6	6-12	12-18	18 hadi Yai la 1	Katika Uzalishaji wa Mayai
Protini ghafi %*	18-20	16-18	15-17	17-18	16-18
Nishati (Nguvu) kcal/kg	2,850	2,850	2,900	2,900	2,900

*Hutegemea ubora wa protini

Kwa kuku wa mayai

Kalsiamu 3% hadi 4%

Asilimia 0.5% ya Fosporasi

Kumbuka kwamba ulaji wa chakula hupungua kadri joto linavyopanda zaidi ya 32°C (90°F) Inaweza kuongezeka ikiwa hali joto ya nje itabakia juu ya 37°C (98°F)



Vitamini na Madini

Vitamini na madini ni muhimu kwa ajili ya ukuaji mzuri wa mifupa na uzalishaji wa mayai. Vyanzo vya vitamini hujumuisha.

Majani mabichi ya mimea, mbegu na matunda.

Vyanzo vya madini hujumuisha

Makaka - maganda ya yai, simbi, makaka ya konokono (yapike na kuyasaga kabala ya kutumia).

Chakula cha mifupa - hutengenezwa kwa kuisaga. Bidhaa za chokaa - chokaa ni chanzo kizuri cha kalsiamu

Nishati

Vifaranga wanahitaji nishati kwa ajili ya kuishi, kukua na kutaga mayai.

Nishati huwasaidia kuku kuwa
wenye nguvu. Nishati hutokana na
vyanzo viwili.

Wanga
Fati na Mafuta



Wanga

Wanga ni chanzo kikubwa zaidi cha nishati kwa ajili ya kuku:

Mahindi
Ulezi
Mtama
Mchele
Viazi vitamu
Mazao ya mizizi na matunda yenye wanga
Mbegu



Fati na Mafuta

Nafaka nyingi zina kiasi cha fati na mafuta.

Vyanzo vingine hujumuisha chakula cha
mbegu za mafuta kama vile

Chakula cha mbegu za soya.
Kiini cha mawese Karanga



Kadiria chakula kinachotumka kila siku (gramu) kwa kuku

Umri (wiki)	Kuku wa Mayai	Kuku wa Kisasa Broila
1	10	21
2	15	50
3	20	95
4	25	135
5	30	170
6	40	190
7	45	200
8	50	
9	55	
10	60	
11	65	
12	70	
13	75	
14	80	
15	85	
16	90	
17	100	
18	105	
19	110	
20	120	
21 na kuendelea	130	

Kadiria maji yanayotumika kila siku unywaji wa maji (ml) kwa kuku

Umri (wiki)	Kuku wa Mayai	Kuku wa Kisasa Broila
1		65
2		120
3		180
4	100	245
5		300
6		330
7		400
8		
9		
10		
11		
12	160	
13		
14		
15		
16		
17		
18	200	
19	220	
20	250	
21 na kuendelea	270	

*Hali ya joto kali itaongeza matumizi ya maji

Tunza Chakula

Chakula kiwe
kikavu muda
wote. Hakikisha
wadudu
waharibifu
hawakifikii,
yaani, panaya na
kadhalika.

Kiinue juu kisikae kwenye sakafu.



Kuchanganya chakula

Tengeneza chakula
chako mwenyewe.
Ni njia ngumu
sana.

Nunua chakula kutoka kwa wauzaji.

Ni njia rahisi kabisa lakini mara zote si bei
rahisi. Changanya chakula ulichokitengeneza
nyumbani pamoja na chakula ulichonunua.

Nunua chakula halafu changanya na nafaka zako au chakula kingine cha
kuongeza nguvu.

